**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA**

SHULE YA SEKONDARI IGUNGA,
S. L. P 169,
**IGUNGA.**

**Kumb Na: IGSS/F5/20/…………** ……./……./2022

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………………..
……………………………………………………………
S.L.P …………………..
…………………………..

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO MWAKA 2022 KATIKA SHULE YA SEKONDARI IGUNGA, HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA, MKOA WA TABORA.**

## 1. UTANGULIZI

Ninafurahi kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2022 Tahasusi ya HGK [ ] HKL [ ] HGE [ ] katika Shule ya Sekondari Igunga.Shule ya Sekondari Igunga ni shule ya bweni kwa wanafunzi wa Kidato cha Tano na cha Sita na ya kutwa kwa wanafunzi wa Kidato cha I-IV.**HONGERA NA KARIBU SANA.**

### 1.1 MAHALI SHULE ILIPO NA JINSI YA KUFIKA

Shule ya Sekondari Igunga inapatikana katika Wilaya ya Igunga, Mkoa wa Tabora.Shule ipo umbali wa kilometa moja na nusu (1.5km) kutoka stendi ya mabasi Igunga.Usafiri wa bajaji na pikipiki maarufu kama bodaboda nauli yake ni Tsh 1000-2000/=.

Muhula wa masomo utaanza tarehe ................ Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ................

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:

### 2.1 SARE YA SHULE

**Wasichana**

- Sketi 2 za rangi ya kijani-jeshi za marinda box (rinda kubwa mbele na nyuma madogo mawili pande zote mbili) zenye urefu wa kufikia katikati ya muundi (chini) isiyobana – kwa Waislamu; kwa wakristo inch 08 kutoka kwenye magoti kwenda chini na isiyo bana.
- Kwa waislamu, nusu kanzu na juba jeupe lishuke mpaka tumboni
- Shati mbili (02) rangi nyeupe mikono mirefu
- Viatu vya ngozi rangi nyeusi vyenye kamba na kisigino kifupi
- Soksi nyeupe (stoking) jozi mbili
- Sweta moja (01) rangi ya kijani-jeshi (mshono wa V kola yake)

**N.B** 1. Aina ya kitambaa cha kushona nusu kanzu na juba; halua nyeupe nzito au tetron nzito nyeupe au kisukari nyeupe nzito.

2. Wanafunzi wa kike hawaruhusiwi kusuka. Hivyo afikapo shuleni awe amekata nywele zake saizi ya kuchana na brashi

**Wavulana**

- Suruali mbili (02) za rangi ya kijani-jeshi, rinda mbili isiwe modo (modal), upana wan inchi 16 chini isiwe chupa
- Shati mbili (02) nyeupe za mikono mirefu
- Viatu vya ngozi rangi nyeusi vyenye kamba na kisigino kifupui
- Soksi nyeusi (fupi) jozi mbili
- Sweta mbili (02) rangi ya kijani-jeshi (mshono V kola)
- Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali

## 2.2 SARE ZA MICHEZO

**Wasichana**

- Raba nyeupe (soksi kijivu – stoking)
- Truck suit 01 rangi ya bluu bahari
- T-shirt nyekundu (jezi ya Manchester moja)

**Wavulana**

- Raba nyeupe (soksi bluu – stoking)
- T-shirt na bukta rangi ya blue – jezi ya Chelsea

## 2.3 NGUO ZA KUSHINDIA

**Wasichana**

- Sketi mbili (02) – 'light blue mshono kama sketi ya darasani
- T-shirt mbili rangi ya njano zenye kola-nyeusi-(Arusha) zinapatikana shuleni

**Wavulana**

- Suruali mbili (02) 'light blue' linda mbili, inchi 16
- T-shirt mbili rangi ya njano zenye kola-nyeusi-(Arusha) zinapatikana shuleni

***ANGALIZO:***

***Sare zote za shule zishonwe na mzazi kabla hajafika shuleni na pia Mwanafunzi anapowasili shuleni awe katika sare za shule ya sekondari Igunga zilizotajwa hapo juu nguo zingine ambazo hazijatajwa hapo juu, haziruhusiwi kwa namna yoyote ile!***

## 3.0 ADA NA MICHANGO YA SHULE

Ada ya shule kwa mwaka ni Tsh 70,000/=, unaweza kulipa kiasi cha Tsh 35,000.00 kwa mhula au kulipa ada yote kwa mara moja.

**(b) Michango mingine inayotakiwa kulipwa na kila mzazi/mlezi ni:**

(i) Shilingi 25,000/- kwa ajili ya ukarabati wa samani.

(ii) Shilingi 6,000/- kwa ajili ya vitambulisho na picha.

(iii) Shilingi 20,000/- kwa ajili ya Taaluma

(iv) Shilingi 30,000/- kwa ajili ya kuwalipa walinzi, wapishi na vibarua wengine

(v) Shilingi 2,000/- kwa ajili ya nembo ya shule.

(vii) Fedha ya tahadhari 5,000/= (Haitarejeshwa)

(viii) Shilingi 10,000/- kwa ajili ya kumkatia CHF

(ix) Shilingi 20,000/- kwa ajili ya mitihani ya Mock kidato cha tano.

**JUMLA YA MICHANGO YOTE NA ADA YA SHULE TSH: 188,000/=**

***Fedha zote zilipwe kwenye Akaunti ya Shule Na 50901100025, IGUNGA SECONDARY RECURRENT katika benki ya NMB ( Tafadhari andika Jina la Mwanafunzi kwenye pay slip)***

## 4. MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI

(i) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
(ii) Scientific calculator kwa wanafunzi wa HGE
(iii) Godoro futi mbili na nusu
(iv) Mashuka pair mbili (02) rangi ya pinki (kwa wasichana) na rangi ya bluu (kwa wavulana), foronya moja(rangi iendane na rangi ya shuka),chandarua (3x3)
(v) Vyombo vya chakula (sahani,bakuli,kijiko na kikombe)
(vi) Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko
(vii) Kwanja 01, jembe 01, mifagio ya ndani(soft broom) na ya nje (hard broom), reki moja (01) na panga (01)
(viii) Picha nne za wazazi/ndugu wa karibu wanaoweza kumtembelea shuleni pamoja na namba zao za simu

## 5.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Namba 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu sayansi na teknolojia ,yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Raisi tawala za mikoa na serikali za mitaa–(TAMISEMI) yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(i) Heshima kwa walimu, viongozi, wafanyakzi wasio walimu, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(ii) Mahudhurio katika shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule,ni lazima
(iii) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
(iv) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo nadi na nje ya mipaka hiyo wakati wote na uanafunzi wako katika shule hii.
(v) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
(vi) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa
(vii) Kutotembelea mabweni yasiyo ya jinsia yako.
(viii) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na
(ix) Kutunza mali za shule

## 6.0 MAKOSA YANAYOWEZA KUKUFUKUZISHA SHULE

***(i) "Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule"***
(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku **90** bila taarifa/utoro
(iii) Kugoma au kuhamasisha mgomo
(iv) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya vikiwemo uvutaji wa sigara, bangi na kubeli.
(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafuzi wenzake,kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule
(vi) Kuharibu kwa makusudi mali ya UMMA
(vii) Kufuga ndevu
(viii) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
(ix) Kudharau wimbo na Bendera ya Taifa.
(x) Uvutaji wa sigara
(xi) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja
(xii) Kupata ujauzito au kutoa mimba
(xiii) Kusababisha au kumpa msichana mimba
(xiv) Kugoma, kuchochea mgomo, kuongoza au kuvunja amani na usalama wa shule.
(xv) Kukataa adhabu kutoka kwa viongozi au walimu.

(xvi) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni

(xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua,au kutishia kujiua kama kunywa sumu, nk

(xviii) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.

(xix) Wizi

## 7.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

(a) "Medical Examination Form" ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya serikali ili kuthibitisha afya yako.

(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafuzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai.

(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria,kanuni, na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YETU.**
**LEONATUS BUSWELU**

.......................................

**MKUU WA SHULE**
(0784905605)

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI IGUNGA
S.L.P. 169
IGUNGA

**KWA MAWASILIANO ZAIDI**
**MWL MICHAEL MATALU (MAKAMU MKUU WA SHULE) 0683062969**

**KIAMBATANISHO A**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IGUNGA SECONDARY SCHOOL**

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

To be completed by a medical officer in respect of all FORM – entrants

Please examine the under mentioned student as to his/her physical and mental fitness for his/her full time student of the school.

Student's name: ……………………………………………………………………………………

Age: …………………………………………………………………………………………………

Blood found (red and white): ………………………………………………………………

Stool examination: …………………………………………………………………………

Urinalysis: …………………………………………………………………………………

Venereal: ……………………………………………………………………………………

Disease / esc:………………………………………………………………………………

TB Test: ……………………………………………………………………………………

Eye Test: ……………………………………………………………………………………

Spleen: ………………………………………………………………………………………

Abdomen: ……………………………………………………………………………………

Urine for pregnant: ……………………………………………………………………

**ABNORMAL INFORMATION** (If any) eg. Physical defects impairment(s) eg. Arm, legs etc. infection chronic or family disease etc……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

I certify that the above is fit to peruse his/her education as stated above.

Signature: ……………………………………………

Designation: …………………………………………

Station: ………………………………………………

Date: …………………………………………………

## KIAMBATANISHO B

## HABARI ZA MWANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi: ...............................................................................................
2. Kabila.......................................................................................................................
3. Tarehe ya kuzaliwa ...................................................................................................
4. Alizaliwa katika Wilaya ya ......................................................................................
5. Dini ..........................................................................................................................
6. Jina la mzazi / mlezi ................................................................................................
7. Anuani kamili ya mzazi / mlezi

   **Mtaa wa ...............................................................**

   **Kijiji cha ...............................................................**

   **Tarafa ...................................................................**

   **Wilaya ..................................................................**

   **Mkoa ....................................................................**

   **S.L.P ....................................................................**

8. Namba ya simu .......................................................................................................
9. Kazi ya mzazi / mlezi ...............................................................................................
10. Taja au eleza juu ya mwanafunzi kama ana ugonjwa wowote unaohitaji uangalizi .........................................................................................................................
11. Taja udhaifu wowote wa mwili au afya alionao mwanafunzi na Uambatanishe cheti cha Daktari anayetambulika ...............................

    ........................................................................................................................

    ........................................................................................................................

    ........................................................................................................................

    ........................................................................................................................

## KIAMBATANISHO C
## AHADI YA KUFUATA SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE (MWANAFUNZI)

Mimi ……………………………………………

Naahidi kufuata sheria, kanuni na taratibu za shule hii na kutekeleza maagizo yote yatakayotolewa na uongozi wa shule wakati wote nitakapokuwa ndani nanje ya shule.

Sitajihusisha na migomo, fujo, wala makosa ya jinai.

Saini……………………………..          Tarehe……………………

**AHADI YA MZAZI/MLEZI**

Mimi ……………………………………….. ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi aliyeweka ahadi hapo juu, naahidi kumpatia ada ya shule, michango na mahitaji yote yanayotakiwa kujiunga na shule hii.

Saini ……………………………………          Tarehe …………………………

**FOMU YA PICHA NNE**

Fomu ya picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni.

| | MZAZI | | | MWANAFUNZI | |
|---|---|---|---|---|---|
| PICHA | | | | | |
| JINA | | | | | |
| ANWANI | | | | | |
| SIMU | | | | | |
| ANAPOISHI | MTAA | TARAFA | WILAYA | | |
| | | | | | |



Shamba dress



Sport dress for girls




Smart dress



Sport dress for boys



Smart dress